FORM FOUR UMEKTA EXAMINATIONS 2023

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA MANISPAA LINDI

# MTIHANI WA UMEKTA KIDATO CHA NNE

**021** **KISWAHILI**

**MUDA: SAA 3** **JULAI 2023**

**MAELEKEZO**

1) Mtihani huu una sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi na moja (11).

2) Jibu maswali yote katika sehemu A na B na **maswali mawili(2)** kutoka sehemu C. Swali la **kumi na moja (11)** ni la lazima.

3) Sehemu A in alama kumi na sita (16), sehemu B in alama hamsini na nne (54) na sehemu C ina alama thelathini (30).

4) Simu ya mkononi na vifaa vyote visivyohusika haviruhusiwi ndani ya chumba cha mtihani.

**SEHEMU A (ALAMA 16)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x), kisha andika herufi ya jibu ilo katika kijitabu cha kujibia

   (i) Kikundi cha maneno kinachoonesha jambo lililotendwa na mtenda katika sentensi hujulikanaje?

   (a) Chagizo

   (b) Kitenzi

   (c) Kivumishi

   (d) Shamirisho

   (e) Nomino

   (ii) "Kushindana na mtu aliyekuzidi kwa kila hali si busara" Methali zifuatazo zinashabihiana na kauli hii isipokuwa;-

   (a) Mwenye pesa si mwenzio

   (b) Nazi haishindani na jiwe

   (c) Chanda chema huvikwa pete

   (d) Mwenye nguvu mpishe

   (e) Maji yakija kasi yapishe

   (iii) Pande mbili zinazohusika latika lugha ya maandishi ni zipi?

   (a) Mwandishi na msikilizaji

   (b) Msikilizaji na msomaji

   (c) Mwandishi na mzungumzaji

   (d) Msomaji na msimuliaji

   (e) Msomaji na mwandishi

   (iv) Fungu la sauti zinazotokea katikati au mwishoni mwa kila mstari wa ushairi huitwaje?

   (a) Vina

   (b) Vituo

   (c) Mizani

   (d) Silabi

   (e) Mistari

   (v) "Juma anaendesha baiskeli yake polepole" kiarifu cha sentensi hii kimejengwa kwa mfuatano upi wa viambajengo?

   (a) Kiima, chagizo na shamirisho

   (b) Kitenzi kishirikishi, shamiirisho na chagizo

(c) Kiarifu, kiima na chagizo

(d) Shamirisho, chagizo na kiteenzi kikuu (e) Kitenzi kikuu, shamirisho na chagizo

(vi) Hamsini, laki, kasri na fikiri ni miongoni mwa maneno yanayothibitisha asili ya Kiswahili ni;- (a) Kiarabu

(b) Krioli

(c) Kibantu

(d) Pijini

(e) Chotara

(vii) "Ni budi nisome kwa bidii ili nifaulu mitihani yangu" Yapi ni masahihisho sahihi ya sentensi hii?

(a) Nina budi kusoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yangu

(b) Sio budi kusoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yangu

(c) Sina budi kusoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yangu

(d) Sitakiwi kusoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yangu

(e) Sio lazima kusoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yangu

(viii) Kipi kati ya vifuatavyo si kipengele kinachopaswa kuzingatiwa wakati wa kutunga igizo?

(a) Uteuzi wa lengo

(b) Uteuzi wa muundo

(c) Uteuzi wa mandhari

(d) Uteuzi wa mizani

(e) Uteuzi wa wahusika [ ]

(ix) Chunguza taarifa ifuatayo, kisha jibu swali linalofuata

Skuli ya sekondari Bandarini

S. L. P 197, Zanzibar.

17/3/2021.

Taarifa hii ina vipengele vingapi?

(a) Kimoja: anwani ya mwandishi

(b) Viwili: anwani ya mwandishi na tarehe

(c) Viwili: anwani ya mwandishi na alama za uandishi

(d) Vitatu: anwani ya mwandishi, mji mdogo aliopo mwandishi na tarehe

(e) Vinne:sehemu mahususi aliyopo mwandishi, sanduku la posta, mji aliopo mwandishi na tarehe

(x) Neno lipi kati ya haya yafuatayo halikuundwa kwa njia ya unyambulishaji?

(a) Wimbo

(b) Kicheko

(c) Mchezo

(d) Chamcha

(e) Kipigo

2. Oanisha maelezo yaliyopo **fungu A** na dhana zilizopo **fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi ili kukamilisha maana

| FUNGU A | | FUNGU B |
|---|---|---|
| (i) | Huandikwa juu kwenye pembe ya upande wa kulia wa karatasi | (a) Barua rasmi |
| (ii) | Wako katika ujenzi wa Taifa | (b) Ndugu |
| (iii) | Hutumia maneno maalumu yenye kuzingatia maadili | (c) Kumbukumbu namba |
| (iv) | Hurahisisha kujua barua iliandikwa lini | (d) Insha |
| (v) | Neno linalosimama badala ya salamu katika barua rasmi | (e) Kimalizio cha barua rasmi |
| (vi) | Hutumika ikiwa barua husika ni mwendelezo wa barua zilizopita na zitakazoandikwa baadaye kuhusu mada ileile na kwa mwandikiwa yule yule | (f) Tarehe |
| | | (g) Barua za kirafiki |
| | | (h) Anwani ya mwandishi |

**SEHEMU B (ALAMA 54)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii

3. (a) Bainisha umbo linalodhihirisha kauli katika maneno yafuatayo kisha taja kauli husika kwa kila neno

(i) Wanapigana

a) Umbo la kauli ________________________

b) Kauli yenyewe ________________________

(ii) Atatusomesha

a) Umbo la kauli ________________________

b) Kauli yenyewe ________________________

(iii) Limelimwa

a) Umbo la kauli ________________________

b) Kauli yenyewe ________________________

(iv) Amesomewa

a) Umbo la kauli ______________________________________________

b) Kauli yenyewe _____________________________________________

(v) Amepigika

a) Umbo la kauli ____________________________________________

b) Kauli yenyewe ___________________________________________

(vi) Amempikia

a) Umbo la kauli ______________________________________________

b) Kauli yenyewe ______________________________________________

(b) Bainisha kiwakilishi katika tungo zifuatazo na kwa kila moja onesha ni kiwakilishi cha aina gani?

(i) Mtoto wangu amerudi, wako hajarudi

(ii) Wengi wamepokelewa vizuri

(iii) Yule hapendi ugali

4. Kwa kutumia mkabala wa kimuundo changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya ngoe

(i) Kuku mweupe amechinjwa asubuhi

(ii) Wanafunzi wote walikuwa wanacheza mpira uwanjani lakini walimu wao waliondoka

5. (a) Unawezaje kuondoa utata katika tungo za Kiswahili? Toa hoja tano (5)

(b) Eleza maana mbili kwa kila tungo (i) Mama anaota

(ii) Tafadhali nipe sahani ya kulia

(iii) Vijakazi wanalima barabara

(iv) Amekanyaga mtoto

6. Ukiwa kama Mtanzania mzalendo unayependa nchi yako eleza namna utakavyoikuza na kuieneza lugha ya Kiswahili nchini na kulinda isitoweke. Toa hoja nne tu.

7. Kwa kutumia mifano kutoka katika riwaya ya Takadini iliyoandikwa na Ben J. Hanson (MBS) eleza kwa kifupi madhara sita (6) yanayoweza kutokea katika jamii iwapo itaendekeza mila potofu kwa kuwabagua walemavu wa ngozi.

8. (a) Eleza tofauti za msingi kati ya barua ya mwaliko na tangazo

(b) Andika tangazo la kumtafuta ndugu yako wa kiume anayeitwa Mabele Madale ambaye amepotea

**SEHEMU C (ALAMA 30)**

Jibu maswali mawili tu kutoka katika sehemu hii. **swali la 11** ni la lazima

9. Waandishi wa riwaya za Watoto wa mama Ntilie na Joka la mdimu wameonesha kuwa rushwa ni miongoni mwa matatizo yanayozikabili jamii nyingi. Kwa kutumia mifano, eleza mambo matatu yaliyopendekezwa kwa waandishi kwa kila riwaya yenye lengo la kuzuia rushwa katika jamii.

10. Chagua mashairi matatu kwa kila diwani mbili ulizosoma kisha onesha jinsi washairi walivyo walimu bora wa jamii.

11. “Tanzania bila fasihi ni sawa na gari bila dereva” Tetea kauli hiyo kwa hoja sita (6)

**ORODHA YA VITABU**

**USHAIRI**

| | |
|---|---|
| Wasakatonge | - M.S Khatibu (Dup) |
| Malenga Wapya | - Takiluki (Dup) |
| Mashairi Ya Chekacheka | - T.A Mvungi (Ep & D.Ltd) |

**RIWAYA**

| | |
|---|---|
| Takadini | - Ben J Hanson (Mbs) |
| Watoto Wa Mama Ntilie | - E. Mbogo (H.P) |
| Joka La Mdimu | - A.J. Safari (H.P) |

**TAMTHILIYA**

| | |
|---|---|
| Kilio Chetu | - Medical Aid Foundation (T[H) |
| Ngoswe Penzi Kitovu Cha Uzembe | - E. Semzaba (Esc) |
| Orodha | - S. Reynoids (Ma) |